**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**CHUO CHA UALIMU SINGACHINI**

Simu: 0753-502082-Mkuu wa chuo
0787304031-Msajili
Barua pepe: singachinitc@moe.go.tz

Chuo cha Ualimu Singachini
S.L.P 586
**MOSHI.**
11 Juni, 2026

Ndugu …………………………………
…………………………………
…………………………………

**FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU ELIMU AWALI NA UALIMU SHULE ZA MSINGI KWA NJIA YA MASAFA (KWA LUGHA YA KISWAHILI) 2026/2027**

**KAULIMBIU YA CHUO**
***"Juhudi na Maarifa ya Kutayarisha Walimu Bora Katika Taaluma, Elimu ya Kujitegemea, Usafi na Nidhamu"***

**1.** Nakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali kwa lugha ya Kiswahili na Stashahada ya ualimu katika shule ya Msingi kwa njia ya masafa, katika Chuo cha Ualimu Singachini mwaka wa masomo **2026/2027.**
Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali ni ya miaka miwili (2) kwa wanachuo wa bweni, miaka mitatu hadi minne (3-4) kwa wanachuo wa mafunzo ya Ualimu kwa njia ya masafa. Mafunzo haya yatakupa mbinu mbalimbali zitakazokuwezesha kufundisha kwa umahiri masomo yanayofundishwa katika shule za awali nchini Tanzania.

**2.** Tarehe ya kuripoti chuoni ni tarehe **17/08/2026.** Tafadhali zingatia tarehe hii kwani usiporipoti kwa wakati ndani ya siku kumi na nne (14) tangu tarehe uliyotakiwa kuripoti utakuwa umepoteza nafasi hiyo.

**3.** Chuo kipo upande wa Kaskazini wa mji wa Moshi wastani wa Kilomita kumi na mbili (12km) kutoka mjini. Mara ufikapo stendi kuu ya mabasi Moshi Mjini, unaweza kutumia njia zifuatazo kufika chuoni;-

i. Panda magari yaendayo **Kibosho-Mweka**, kisha mkumbushe **Kondakta** akushushie kituo cha **Kibaoni Nauli ni Tsh. 1000/=,** hapo utaona kibao kinachokuelekeza barabara ya magari ya vumbi inayoingia kushoto ifuate kisha ukishavuka daraja fuata barabara ya mkono wa kushoto itakayokufikisha chuoni umbali wa kilometa 1.5 **au**

ii. Panda magari yaendayo **Kibosho-Kirima**. kisha mkumbushe **Kondakta** akushushie kituo cha **Kirima Chini KNCU**, hapo utaona kibao kinachokuelekeza njia ya miguu ya kufika Chuo cha Ualimu Singachini. Nauli kwa njia hii ni **Tsh. 2000/=**

iii. Usafiri wa Taxi itakayokuleta moja kwa moja hadi chuoni kwa **njia ya Kibosho-Mweka** kupitia **KCMC** ni kati ya **Tshs. 12,000/=** na **15,000/=** (Itategemea maelewano yako na mwenye Taxi).

**4. Unahitajika kuja na mahitaji yafuatayo:**

**(i) Sare ya Chuo**

**Wavulana**:

Mashati 2 ya mikono mirefu ya bluu bahari (**Light Blue**), Suruali 2 nyeusi za kushona zisizo za kubana wala mifuko miwili nyuma (upana wa chini usipungue inchi 15), viatu vyeusi vyenye kamba na soksi nyeusi; tai nyeusi yenye mistari myeupe (hii utanunua mjini baada ya kufika chuoni, andaa shilingi 5,000/=), T-shirt yenye nembo ya chuo *(hii inapatikana chuoni andaa shilingi 15,000/=)*

**Wasichana:**

Sketi 2 nyeusi ndefu hadi chini ya goti zenye rinda la **"V",** mashati 2 ya mikono mirefu ya bluu bahari (**Light Blue**), tai nyeusi yenye mistari myeupe (hii utanunua mjini baada ya kufika chuoni, andaa shilingi 5,000/=), T-shirt yenye nembo ya chuo *(hii inapatikana chuoni andaa shilingi 15,000/=)*, viatu vyeusi vyenye kamba na soksi nyeupe. Angalia kwa makini rangi za vitambaa ili kupata rangi inayohitajika. ***(****Endapo hutakuwa na uhakika wa rangi halisi ya kitambaa, unashauriwa kununua sare baada ya kufika chuoni ili uweze kupata rangi halisi za vitambaa vya sare****).*** Sare hii iwe ya heshima isiwe ya kubana, marembo au madoido yeyote yasiyo ya msingi.

Kila mwanachuo aje na sweta ya rangi ya **Dark-Blue** ya mikono mirefu pamoja na koti **jeusi** la suti linaloendana na kitambaa cha rangi ya suruali au sketi kwa kwa ajili ya kuvaa wakati wa baridi. **Hii ni kwa wote, Wavulana na Wasichana).**

Aidha wanachuo wa kike wa Dini ya Kiislamu (kwa wale watakaopenda) wanaweza kuvaa:-**"Short Kanzu" 2** za rangi ya bluu bahari **(Light blue)** badala ya shati zinazokaribia kwenye magoti, hijabu ya bluu bahari **(Light blue)** iliyoshonwa mtindo wa Juba/ Shungi, sketi nyeusi 2 **ndefu hadi chini** zenye rinda la **"V".** *Hata hivyo bado inaruhusiwa kuvaa sare kama wasichana wengine.*

**(ii) Mavazi mengineyo**

Mavazi mengine yawe nadhifu na ya heshima yanayoendana na hadhi ya kazi ya Ualimu. Unakumbushwa kuja na jacket au sweta nzito kwa ajili ya kujikinga na baridi nyakati za usiku kwa kuwa ukanda huu ni wa baridi.

**(iii) Sare ya michezo:**

Wavulana-Bukta na T-shirt ya rangi ya **BLUU (Jezi ya Chelsea)** Wasichana-Bukta (P.T Shorts) na T-shirt rangi ya **BLUU**. Wote waje na raba au viatu vya michezo, soksi (stockings) rangi ya bluu na ***Track Suit rangi ya dark bluu***. *Zingatia sare zote zitakaguliwa wakati wa kuripoti chuoni*.

Michezo inayochezwa hapa chuoni ni pamoja na mpira wa miguu, mpira wa mikono, mpira wa pete, mpira wa wavu, mpira wa kikapu, mpira wa meza, riadha na fani za ndani.

**(iv) Vifaa vya kulalia:**

Wasichana: Shuka 2 rangi ya **Pinki**, blanketi, mto na foronya. Chandarua rangi nyeupe kwa ajili ya kijikinga na mbu.

Wavulana: Shuka 2 rangi ya **Bluu bahari**, blanketi, mto na foronya, chandarua rangi nyeupe.

**(v) Vifaa vya Darasani**:

Daftari kubwa (counter book) zisizopungua 10 zenye kurasa si chini ya 96, marker pen dazeni 1, mkasi mdogo, rangi za maji za kuchorea seti 1, rula, mkebe wa Vifaa vya Jometri, karatasi nyeupe **photocopier** rimu 1 aina ya ***Paperline Original*** (kwa muhula) kwa ajili ya kazi za mazoezi mbalimbali darasani. (Vifaa hivi ni muhimu sana kwa ajili ya mafunzo ya ualimu).

**(viii) Vifaa vya chakula:** Kijiko, kikombe, sahani ya **udongo** au **mfupa** na Thermos ukipenda.

**(ix) Vifaa vya usafi:** Ndoo 1 ya ujazo wa lita 20 kwa shughuli za usafi.

**5. MAAGIZO MENGINEYO**

(i) Mwanachuo awe na fedha za matumizi binafsi na mahitaji madogomadogo chuoni.

(ii) Unalazimika kupimwa na Daktari anayetambuliwa na Serikali ili kuthibitisha afya yako ya kumudu mafunzo haya. Imeambatanishwa fomu ya kupimwa utakayoiwasilisha chuoni wakati wa kuripoti.

(iii) Mwanachuo ataelekezwa sheria na taratibu za chuo afikapo chuoni,aidha,atapewa fomu ya kujaza kukubaliana na sheria na taratibu za chuo.

(iv) BIMA YA AFYA (NHIF) kwa ajili ya matibabu yako yote (Bima hii ni **lazima** kwa kila mwanachuo). Chuo kinatoa huduma ya kwanza tu. Kwa ambaye **hana** anashauriwa kutembelea ofisi za bima ya afya zilizopo kwenye maeneo unapotoka ukiwa na namba ya NIDA. Kwa mwanachuo Bima ya Afya inapatikana kwa gharama ya sh. 50,400/=

**6. ADA NA MICHANGO WANACHUO WA KAWAIDA**

***(a)*** **Ada ya Mafunzo** kwa mwaka ni Tshs. **450,000/=** .Inaweza kulipwa yote au kwa awamu mbili Tshs. **225,000/=** kwa kila muhula. ***Fedha hii ya ada italipwa benki (NMB au NBC au CRDB) baada ya mwanafunzi kupata namba ya utambulisho (Control number) ya mfumo wa malipo ya serikali kutoka kwa mhasibu wa chuo. (wasiliana na mhasibu kwa namba 0757197584 ili kupata control number).***

(b) **Michango mingine**

| NA. | MCHANGO | KIASI | MAONI |
|---|---|---|---|
| 1. | Serikali ya Wanachuo | 5,000/= | Kwa Mwaka |
| 2. | Huduma ya Kwanza | 10,000/= | Kwa Mwaka |
| 3. | Usafi na Mazingira | 20,000/= | Kwa Mwaka |
| 4. | Kukodisha godoro | 10,000/= | Kwa Mwaka |
| 5. | Usajili na Kitambulisho | 20,000/= | Kwa Mwaka wa Kwanza tu |
| 6. | Michezo | 30,000/= | Kwa Mwaka |
| 7. | Ulinzi | 30,000/= | Kwa Mwaka |
| 8. | Ukarabati | 25,000/= | Kwa Mwaka |
| 9. | Bima ya afya **(NHIF)** | 50,400/= | Kwa Mwaka (Kwa asiye na Bima) |
| | **JUMLA** | **200,400/=** | |

c) **ADA NA MICHANGO YA MWANACHUO WA STASHAHADA YA UALIMU KWA NJIA YA MASAFA** kwa walimu kazini ni Tsh **450,000** ada na **150,000 kama michango kwa ajili ya gharama za uendeshaji.**
Michango **yote** ilipiwe katika Tawi lolote la **NBC** lililopo karibu nawe. Tumia Namba ya Akaunti Ifuatayo: NBC **AC. NO. 017101006490** SINGACHINI COLLEGE OF EDUCATION, Uje na *Pay- In-Slips* halisi (Originals) na nakala (copy) ulizolipia ada na michango zenye majina yako kamili na zinazoonesha Jumla ya kiasi cha Ada na Michango uliyolipa. ***Fedha taslimu haitapokelewa***.

**Angalizo:**

a) Ada zote hulipwa kwa namba maalumu ya utambulisho (Control Number), usilipe fedha ya ada kwenye akaunti ya michango.

b) Michango yote hulipwa kupitia akaunti ya **NBC** iliyotajwa.

c) Yeyote atakayeshindwa kuja na kiasi kilichoagizwa **hatapokelewa**. Aidha, ***fedha ikishalipwa kwenye akaunti ya serikali haitarudishwa.***

**7.** Chuo kinatoa chakula kulingana na utaratibu uliopangwa, hakitoi *Chakula Maalum* **(Special Diet)** kabisa; pia hairuhusiwi kwa mwanachuo yeyote kujipikia chakula chake binafsi hapa chuoni.

**8. VYETI**

Uje na **VYETI HALISI (ORIGINAL CERTIFICATES**) na **VIVULI (PHOTOCOPIES)** vya vyeti vifuatavyo:-

(i) Cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne na Sita (School Leaving Certificate).

(ii) Cheti cha kufaulu Kidato cha Nne na Sita (Academic certificate). Hati ya matokeo (Results Slip) haitapokelewa kwa wale ambao vyeti halisi tayari vilishatolewa na baraza la mitihani Tanzania.

(iii) Ikiwa ulisharudia Mtihani wa kidato cha Nne au cha Sita,au kusoma kozi ya ualimu huko nyuma hakikisha kuwa **unakuja na cheti/vyeti husika**, hata kama ulifeli mitihani hiyo hakikisha unakuja na taarifa husika za mtihani/mitihani hiyo.

(iv) Cheti cha kuzaliwa.

(v) Kitambulisho cha NIDA.

**NB: Zingatia maelekezo ya vipengele vyote kikamilifu kwani usipotimiza maelekezo hautasajiliwa .**

*KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU SINGACHINI*

**URLICK M. NDUNGURU**

**MKUU WA CHUO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU
SINGACHINI
P. O. Box586-MOSHI

# GOVERNMENT OF TANZANIA
## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

TO: The Medical Officer From: **Singachini Teachers' College**

…………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teachers course.

A: 1. (a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases.

B: Blood Group………………………………………………………………..

Date:…………………………………………………………… Signature:………………………………………
Official Stamp

**************************************************************************************

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full time Teacher Education Course.

- (a) Eye – sight ……………………………………………………………………………..
- (b) Hearing……………………………………………………………………………………..
- (c ) Limbs………………………………………………………………………………………..
- (d) Speech……………………………………………………………………………………
- (e) Leprosy……………………………………………………………………………………..

II. Neuroses …………………………………………………………………………………………….
III. Other serious diseases………………………………………………………………………..
IV. Pregnancy ……………………………………………………………………………………………

**Date: …………………………………………………………. Signature: ……………………………………………………………………..**

**Official Stamp**